Government of **Western Australia**
Department of **Health**
Public and Aboriginal Health Division

Mpango wa Kidato cha 10 wa Uchanjo wa Meningococcal ACWY kwa Shuleni 2019

Ugonjwa wa meningococcal ni nini?

Ugonjwa wa meningococcal ni ugonjwa ambao si kawaida, lakini unaweza kutisha uhai. Ugonjwa husababishwa na maambukizo ya bakteria ya damu na/au utando unaoweka ndani uti wa mgongo na ubongo.

Ingawa unaweza kutibiwa na kiua vijasumu, maambukizo yanaweza kuendelea upesi sana, kwa hiyo ni muhimu kwamba yeyote anayepata dalili za ugonjwa wa meningococcal atafute tiba ya uganga upesi.

Katika wakati wowote, karibia asilimia 10 ya watu wenye afya wanakuwa na bakteria ya meningococcal bila kuumizwa puani au imo koo, na haumwi.

Je, unapata ugonjwa wa you get meningococcal njia gani?

Bakteria ya meningococcal inaenezwa na utemaji wa pumzi (kukohoa, kupiga chafu au kubusu). Bakteria haiishi kwa zaidi ya sekondi chache katika mazingira.

Ugonjwa unawezekana sana kueneza tu kwa watu wa karibu sana, kama watu wanaoishi kwenye nyumba pamoja, wenzi na watoto wanaoenda kituo kilekile cha utunzaji wa siku kwa zaidi kwa masaa manne yanayofuatana.

Mbona WA Health inatoa programu ya uchanjo kwa wanafunzi wa Kidato cha 10?

Karibuni maambukizo ya meningococcal yamezidi kusababishwa na aina maalum ya bakteria, ‘serogroup W’.

Ugonjwa wa meningococcal unaweza kuathirika watu wa kundi lolote la umri. Hata hivyo, baadhi ya kiwango cha juu sana ya kubeba na meningococcal na ugonjwa wake unatokea kwa vijana na kundi la umri huu linaweza kueneza kwa watu wanaokuwa na hatari zaidi ya kuambukizwa, pamoja na watoto wadogo.

Inatazamiwa kuwa kuchanja wanafunzi wa Kidato cha 10 kutapunguza kueneza bakteria kwa wengine na kusaidia kuzuia maambukizo katika jumuiya.

Chanjo ipi itatumiwa na inafaa kiasi gani?

Chanjo ya meningococcal ACWY itatumiwa. Chanjo hii inalinda kupinga vikundi vinne serogroups vya Bakteria ya meningococcal: A, C, W na Y. Chanjo ya aina Nimenrix® kitatumiwa na mpango wa kuwemo shule.

Chanjo hiyo ni salama na kufaa. Mipango ya chanjo ya meningococcal ACWY imetekelezwa kwa vijana wenye umri wa miaka 13–15 nchini UK tangu 2015 na vijana wenye umri wa miaka 11–12 nchini US tangu 2005 bila matatizo kutaarifiwa. Chanjo inapewa kawaidia kama kipimo kimoja. Vipimo zaidi vinasifiwa kwa wale wenye hatari zaidi ya kupata ugonjwa na wale wanaosafiri mahali panapo ugonjwa huu ni kawaidia. Utafiti umeonyesha kwamba chanjo ya meningococcal ACWY inaweza kufaa kwa katikati asilimia 80–85 kwa vijana.

Nani asipate chanjo hiii?

Mwambie mtu anayetoa chanjo ikiwa:

- **Una mzio mkali wowote unaotisha maisha.**

  Ikiwa unakuwa na athari ya mzio ya kutisha-maisha baada ya kipimo cha zamani cha chanjo ya meningococcal ACWY, au ukiwa na mzio mkali kwa sehemu yoyote ya chanjo hii, usipate chanjo hiii.

  Mtoaji wako anaweza kukuambia kuhusu viambato vya chanjo.

- **Wewe ni mjamzito au kumnyonyesha mtoto.**

  Chanjo ya meningococcal haipendekezwi kawaidia kwa wanawake wenye mimba au wanamwonyonyesha lakini inaweza kupewa wakati inayohitajika kwa utabibu. Uzungumze zaidi na GP yako kama ungeweza kuwa mjamzito au kama unanyonyesha.

Madhara ya chanjo ni nini?

Kutumia dawa yoyote, pamoja na chanjo, inawezekana kuna madhara mabaya ya kawaida. Haya kawaida ni madogo na yanatoka yenyewe. Athari mkali inawezekana pia, lakini ni adimu. Kunawezekana kidogo sana cha chanjo kusababisha jeraha kali au kifo. Huwezi kupata maambukizo ya meningococcal kutoka chanjo.

Madhara mabaya ya kawaida ni pamoja na maumivu, unyekundu na kuvimba mahali pa kuchanja, homa, kusumbuliwa upesi, uchovu, upungufu wa hamu, maumivu kichwani, upele na kichefuchefu. Hata hivyo, madhara makali mabaya ya jumla ni adimu.

Usalama wa chanjo unaangaliwa kila mara. Kwa habari zaidi, tembelea: www.tga.gov.au au www.immunise.health.gov.au

Nifanye nini kama kuna madhara makali – niangalie nini?

Angalia kwa yoyote inayosababisha wasiwasi kwako, kama dalili za athari mkali ya mzio, homa kali sana, au matendo ambayo si kawaida. Dalili kali za mzio zinaweza kuwa pamoja na mizinga, uvimbe wa uso na koo, ugumu wa kupumua, mapigo upesi ya moyo, kizunguzungu, na udhaifu – kawaida katika dakika chache hadi masaa machache baada ya chanjo. Kwa madhara makali yoyote, piga simu kuita ambulensi au enda kwa idara yako ya karibu sana ya dharura.

Nifanye nini?

Paracetamol inaweza kusaidia kupunguza homa ndogo au maumivu na kitambaa cha baridi chenye maji kinaweza pia kupunguza maumivu palepale mahali pa kuchanja. Utafute ushauri wa uganga au enda kwa idara ya dharura ya mtaani kama unapata athari yoyote unayofikiri ni mkali au hukutazamia.

Au pigia simu ***healthdirect Australia*** kwenye 1800 022 222.

Athari itolewe ripoti kwa Uchunguzi ya Usalama wa Chanjo cha Australia ya Magharibi (WAVSS). Mtoaji wako wa chanjo uweke ripoti hii, au unaweza kufanya wewe wenyewe kupitia tovuti ya WAVSS www.wavss.health.wa.gov.au au 9321 1312

2.30 asubuhi hadi 10.30 mchana (8.30am–4.30pm) siku za wiki.

Habari zaidi

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu chanjo ya meningococcal, wasiliana na ***healthdirect Australia*** kwenye 1800 022 222 au mtoaji wako wa mtaani kwa kutumia habari za kuwasiliana zinatolewa nyuma ya bahasha inayokuwa karatasi yako ya kukubali ndani.

HealthyWA
healthywa.wa.gov.au

Hati hii inaweza kupatikana kwa muundo mbadala ukiomba kwa mtu mwenye ulemavu

Kutengenezwa na Communicable Disease Control Directorate
© Idara ya Afya 2019

Hakimiliki ya mambo hayo ni ya Jimbo la Australia ya Magharibi ila tu ikionyeshwa tofauti. Badala ya matumizi yoyote ya usawa kwa malengo ya masomo ya kinafsi, criticism au kukagua, kama yalivyoruhusiwa chini ya *Sheria ya Hakimiliki ya 1968*, hakuna sehemu inayoweza kutolewa tena au kutumiwa kwa malengo yoyote bila kibali kilichoandikwa mapema kutoka kwa Jimbo ya Australia ya Magharibi.

IMM-013356 JUN'19